# MWONGOZO WA WATAZAMAJI WA NDANI NA WA KIMATAIFA WA UCHAGUZI, 2020

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI
TANZANIA

## YALIYOMO


1.0 Utangulizi ........................................................................ 1

2.0 Jina la Mwongozo na Matumizi.................. 1

3.0 Tafsiri................................................................ 2

4.0 Madhumuni ya Mwongozo kwa Watazamaji...5

5.0 Mwaliko na Usajili wa Watazamaji...................... 5

5.1 Mwaliko............................................................ 5

5.2 Usajili wa Watazamaji......................................7

6.0 Muda wa Utazamaji...................................... 8

7.0 Taarifa na Maelezo Mafupi kwa Watazamaji wa Uchaguzi............................ 8

8.0 Wigo wa Utazamaji................................................... 9

9.0 Haki za Watazamaji....................................... 11

10.0 Wajibu wa Watazamaji.............................................12

11.0 Utaratibu wa kutoa Taarifa................................... 15

12.0 Maelekezo Mengine ya ziada kwa Watazamaji wa Kimataifa............................. 15

13.0 Kanuni za Maadili kwa Watazamaji.............16

14.0 Tamko la Kuzingatia Mwongozo wa Watazamaji ................................................ 18

15.0 Kubatilishwa kwa Usajili wa Mtazamaji....................................................18

16.0 Kufuta Maelekezo kwa Waangalizi ya Mwaka 2015........................................................ 20

## 1.0 Utangulizi

1.1 Ibara ya 74(6) (b) na (d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inaipa Tume ya Taifa ya Uchaguzi mamlaka ya kusimamia na kuratibu uchaguzi wa Rais na Wabunge katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na uchaguzi wa Madiwani kwa Tanzania Bara. Kifungu cha 63(4) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 kinaipa Tume mamlaka ya kuaandaa mwongozo wa watazamaji.

1.2 Ili kufanikisha utekelezaji wa jukumu hilo kwa uwazi, uadilifu na kuhakikisha uwepo wa uwajibikaji wa kutosha, Tume hualika na kutoa vibali kwa mashirika na taasisi za ndani na za kimataifa kutazama uchaguzi.

## 2.0 Jina la Mwongozo na Matumizi

2.1 Mwongozo huu utaitwa **"Mwongozo wa Watazamaji wa Ndani na wa Kimataifa wa Uchaguzi wa mwaka**

**2020"** na utatumika kwa watazamaji watakaopata kibali cha kuwa watazamaji wa uchaguzi wa Rais na Wabunge katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na uchaguzi wa Madiwani kwa Tanzania Bara.

2.2 Mwongozo huu utasomwa pamoja na sheria nyingine za uchaguzi na kanuni zake, ikiwa ni pamoja na Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge na Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za mwaka 2020.

## 3.0 Tafsiri

Katika Mwongozo huu, isipokuwa muktadha utaelekeza vinginevyo-

"Afisa Mwenye Mamlaka" maana yake ni Msimamizi wa Uchaguzi, msimamizi wa kituo, au afisa yeyote aliyeajiriwa na Tume;

"Tume" maana yake Tume ya Taifa ya Uchaguzi;

"Utazamaji wa Uchaguzi" maana yake ni utazamaji wa uchaguzi katika hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi unaofanywa na mtazamaji aliyepata usajili rasmi kwa ajili ya kutekeleza kusudi hilo;

"mtazamaji wa uchaguzi" ni pamoja na mtazamaji wa ndani au wa kimataifa;

"watazamaji wa kimataifa" ni pamoja na-

(a) wawakilishi wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa;

(b) Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(c) Umoja wa Afrika;

(d) Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika;

(e) Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola;

(f) Jukwaa la Tume za Uchaguzi za nchi za Jumuiya ya Maendeleo za Kusini mwa Afrika;

(g) Shirika lolote la Kimataifa linalotambuliwa na Mashirika Wakilishi, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, yanayofanya kazi nchi za nje;

(h) Serikali za nje zilizo na misheni za kidiplomasia nchini au la; na

(i) Shirika lolote la kimataifa linalotambuliwa na lililoomba na kukubaliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuwa mtazamaji wa uchaguzi.

"watazamaji wa ndani" ni pamoja na-

(a) asasi iliyoundwa mahsusi kwa ajili ya utazamaji;

(b) asasi za kiraia ikiwa ni pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali; na

(c) mashirika ya kidini.

## 4.0 Madhumuni ya Mwongozo kwa Watazamaji

Madhumuni ya Mwongozo wa watazamaji ni kutoa-

(a) mwongozo wa namna ya utoaji vibali;

(b) kutambua haki, wajibu na mwenendo wa watazamaji wa ndani na wa kimataifa wakati wa uchaguzi; na

(c) kuweka miongozo ya namna ya kutekeleza masharti na kufuatilia mienendo ya watazamaji wakati wa mchakato wa uchaguzi.

## 5.0 Mwaliko na Usajili wa Watazamaji

### 5.1 Mwaliko

(a) Tume inaweza kutoa mwaliko kwa-

(i) watazamaji wa ndani kupitia vyombo vya habari vya ndani kwa lengo la kuwaalika watazamaji wa ndani kuomba

usajili wa kushiriki katika utazamaji wa uchaguzi; na

(ii) watazamaji wa kimataifa kupitia Wizara inayohusika na Masuala ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kujumuika kama Watazamaji wa Uchaguzi, baada ya kusajiliwa;

(b) Asasi au Serikali zinazotoa ufadhili zinapaswa kuijulisha Tume nia au mipango yao ya kuleta watazamaji wa ndani au wa kimataifa na kutuma maombi kwa ajili ya uthibitisho; na

(c) Tume mara baada ya kupokea maombi, inaweza kukataa au kukubali kutoa kibali cha utazamaji kama itakavyoona inafaa. Hivyo-

(i) pale ambapo Tume itakubali maombi ya kuwa watazamaji itamjulisha mwombaji na kumpatia kitambulisho cha utazamaji; na

(ii) pale ambapo Tume itakataa maombi ya kuwa watazamaji wa uchaguzi, itamjulisha mwombaji.

**5.2 Usajili wa Watazamaji**

(a) Tume itatoa barua rasmi ya uthibitisho kwa asasi na taasisi zilizopata kibali cha utazamaji wa uchaguzi;

(b) kila mtazamaji wa ndani au wa kimataifa atatakiwa kuwasilisha Tume hati zake na wasifu wake kabla ya kupata uthibitisho;

(c) mtazamaji atapewa barua rasmi ambayo ataiwasilisha kwa Msimamizi wa Uchaguzi wa jimbo husika na kupatiwa kitambulisho ambacho

atapaswa kukivaa wakati wote atakapokuwa akifanya shughuli za utazamaji chini ya Mwongozo huu.

**6.0 Muda wa Utazamaji**

Muda wa utazamaji utakuwa kama ifuatavyo-

(a) utazamaji wa uchaguzi utaanza rasmi kuanzia tarehe ya kupata usajili hadi tarehe itakayooneshwa kwenye kitambulisho cha usajili cha mtazamaji; na

(b) Tume inaweza kuongeza muda wa utazamaji wa uchaguzi baada ya kupokea maombi ya kufanya hivyo kutoka kwa asasi au taasisi husika.

**7.0 Taarifa na Maelezo Mafupi kwa Watazamaji wa Uchaguzi**

Tume inaweza kuwapatia watazamaji wa uchaguzi taarifa za awali juu ya masuala ya uchaguzi. Taarifa hizo ni pamoja na-

(a) sheria na kanuni za uchaguzi;

(b) mchakato na taratibu za uchaguzi;

(c) Mwongozo wa Watazamaji;

(d) orodha ya halmashauri, majimbo ya uchaguzi na vituo vya kupigia kura;

(e) orodha ya vyama vya siasa vilivyosajiliwa; na

(f) taarifa nyingine yoyote ambayo Tume itaona ni ya muhimu.

## 8.0 Wigo wa Utazamaji

Mtazamaji wa ndani au wa kimataifa atatazama na kutathmini yafuatayo-

(a) uadilifu wa Tume katika mchakato wa uchaguzi;

(b) maamuzi yanayotolewa na Tume kuhusiana na migogoro ya uchaguzi kama yanafuata kanuni na taratibu na bila kuegemea upande wowote; na

(c) michakato na taratibu za uchaguzi ambazo zinahusisha-

(i) ugawaji wa vituo vya kupigia kura;

(ii) kutangaza kalenda ya uchaguzi;

(iii) utayarishaji na usambazaji wa vifaa vya kupigia kura;

(iv) utoaji wa elimu ya mpiga kura unaofanywa na Tume na Asasi za Kiraia;

(v) mchakato wa kampeni na mwenendo wa vyama vya siasa kwa kuzingatia Maadili ya Uchaguzi;

(vi) matumizi ya vyombo vya habari kwa wagombea na vyama vya siasa;

(vii) wajibu wa vyombo vya habari juu ya usambazaji wa taarifa zilizo za haki na kwa usawa juu ya shughuli na mchakato wa uchaguzi;

(viii) kupiga, kuhesabu, kujumlisha kura na kutangaza matokeo;

(ix) usiri wa kura, uwazi na uhalali wa mchakato wa uchaguzi;

(x) ushirikishwaji katika mchakato wa uchaguzi;

(xi) wajibu wa vyombo vya usalama; na

(xii) taratibu za kutatua migogoro zilizopo katika mchakato wa uchaguzi.

## 9.0 Haki za Watazamaji

Kwa kuzingatia sheria za uchaguzi, watazamaji wa uchaguzi wanaweza-

(a) kuomba na kupatiwa taarifa za msingi kuhusiana na mchakato wa uchaguzi kama inavyoelekezwa katika kipengele cha 8 (c) cha Mwongozo huu;

(b) kutazama hatua za uchaguzi zilizotajwa katika kipengele 8(c);

(c) kuwa na uhuru wa kuzunguka maeneo yote waliyoruhusiwa na Tume kutazama uchaguzi;

(d) kuwasiliana na chama chochote cha siasa; na

(e) kuwepo kwenye vituo vya kupigia kura na kutazama mchakato wa upigaji na uhesabuji wa kura.

## 10.0 Wajibu wa Watazamaji

(a) kuheshimu na kutii Sheria za Tanzania;

(b) kufuata maelekezo yote yatakayotolewa na Tume katika kipindi chote cha utazamaji;

(c) kutofanya jambo lolote ambalo litaingilia masuala ya ndani ya nchi;

(d) kutekeleza wajibu wao kwa uadilifu, uhuru na usawa;

(e) kuitaarifu Tume mgongano wowote wa kimaslahi alionao kuhusiana na mchakato wa uchaguzi;

(f) kuhakikisha kwamba utazamaji ni huru na unafanywa kwa usawa, usio na uelekeo wa kisiasa, na unafanywa kwa umakini na usahihi;

(g) kuepuka kuingilia zoezi la uchaguzi au kwa namna yoyote kuwaelekeza watendaji namna ya kutekeleza majukumu yao;

(h) kuwasilisha taarifa zao au malalamiko yao Tume kwa njia ya maandishi juu ya dosari zozote zitakazojitokeza katika uchaguzi;

(i) kuepuka kuingilia au kudharau majukumu ya watendaji wa uchaguzi;

(j) kufuata maelekezo ya Tume yanayokataza na kuzuia matumizi ya chombo chochote kinachoweza kunasa sauti au kurekodi picha mjongeo; vyombo hivyo vinaweza

kuhusisha simu za viganjani, kamera, vinasa sauti, kamera za video na mawasiliano ya simu ya upepo ndani ya vituo vya kupigia kura;

(k) kutotoa maoni yoyote kwenye vyombo vya habari yanayohusiana na uchaguzi kabla zoezi la uchaguzi kumalizika;

(l) kutokufanya majukumu ya kiutendaji au kujifanya kuwa kamisheni ya uchunguzi;

(m) kuwasilisha taarifa ya utazamaji ndani ya muda ulioainishwa kwenye kipengele cha 11.0;

(n) kurudisha kadi ya utambulisho wa mtazamaji, barua ya utambulisho ya utazamaji na kifaa kingine chochote kilichotolewa kwa mtazamaji pale anapoamriwa na Tume kufanya hivyo; na

(o) Kutumia ujuzi na uelewa wa viwango vya kimataifa katika kutathmini mchakato wa uchaguzi ulio huru na wa haki.

## 11.0 Utaratibu wa Kutoa Taarifa

Watazamaji watawasilisha nakala zao za ripoti ya utazamaji kwa Tume katika kipindi kisichozidi miezi miwili tangu tarehe ya kutangazwa matokeo ya uchaguzi.

## 12.0 Maelekezo mengine ya ziada kwa Watazamaji wa Kimataifa

Mtazamaji wa kimataifa atatakiwa-

(a) kuwa na viza hai ya kuingia nchini;

(b) kuzingatia kanuni za afya kama zitolewavyo na mamlaka husika;

(c) kuzingatia dondoo za kiafya kama zitakavyotolewa na Tume ; na

(d) kuzingatia tahadhari za kiusalama zitolewazo na Tume au vyombo vingine vya utekelezaji wa sheria.

## 13.0 Kanuni za Maadili kwa Watazamaji

Watazamaji wote watapaswa kuzingatia Maadili yafuatayo-

(a) kutii sheria zote za nchi na kanuni zake;

(b) kuimarisha nidhamu na fikra huru;

(c) uaminifu na uhuru wa mawazo;

(d) kuzingatia uadilifu na usawa wa hali ya juu;

(e) kutokutoa maoni yoyote kwa vyombo vya habari juu ya mchakato wa uchaguzi wakati zoezi la upigaji kura linaendelea;

(f) kutotoa taarifa kwa umma juu ya mchakato wa uchaguzi mpaka taarifa ya awali ya utazamaji wao

itakapokuwa imekabidhiwa kwa Tume na Tume kukiri kuipokea, ikizingatiwa kwamba, taarifa kwa umma itakayotolewa haitahusisha matokeo ambayo hayajatangazwa rasmi;

(g) kutofanya majukumu ya kiutendaji au kujifanya kama kamisheni ya uchunguzi;

(h) kutoingilia mchakato wa uchaguzi katika hatua yoyote ya uchaguzi;

(i) kuepuka kufanya kazi kama mwangalizi katika mchakato wa uchaguzi; na

(j) kurejesha nyaraka za utambulisho zilizotolewa na Tume au nyaraka nyingine zozote ambazo zitatakiwa kurejeshwa.

**14.0 Tamko la kuzingatia Mwongozo wa Watazamaji**

Tamko la kuzingatia Mwongozo wa Watazamaji litakuwa kama ifuatavyo-

(a) kila shirika au taasisi inayotarajia au mwakilishi anayetarajia kusajiliwa na Tume kutazama mchakato wa uchaguzi, atapewa nakala ya Mwongozo;

(b) mtazamaji aliyepewa nakala ya Mwongozo huu atatakiwa atoe tamko kwa namna iliyoainishwa kwenye Fomu iliyopo katika Jedwali la Mwongozo; na

(c) mtazamaji atakayeshindwa kufuata Mwongozo huu, Tume itamfutia usajili wa kuwa mtazamaji wa mchakato wa uchaguzi.

**15.0 Kubatilishwa kwa usajili wa mtazamaji**

**15.1** Mtazamaji ataweza kupoteza sifa ya utazamaji wa uchaguzi endapo-

(a) atashindwa kufuata Mwongozo huu;

(b) atakiuka sheria za uchaguzi;

(c) atakiuka sheria na taratibu za uhamihaji;

(d) atakiuka sheria yoyote ya Jamhuri ya Muungano;

(e) atafanya kampeni au kuonesha upendeleo kwa mgombea yeyote au chama cha siasa cha mgombea; na

(f) atakiuka maelekezo mengine yoyote kama yatakavyotolewa na Tume au Mkurugenzi wa Uchaguzi.

**15.2.** Mtazamaji yeyote au taasisi ambayo itakiuka kipengele chochote cha Mwongozo huu au sheria za nchi haitaweza kuwa mtazamaji katika chaguzi za siku zijazo.

## 16.0 Kufuta Maelekezo kwa Waangalizi ya mwaka 2015

Maelekezo kwa Waangalizi wa Ndani na wa Kimataifa ya mwaka 2015 yanafutwa.

## JEDWALI

FOMU YA TAMKO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**Fomu ya Tamko kwa Mtazamaji**

*(Imetolewa chini ya kipengele cha 14(b))*

Nimesoma na kuuelewa Mwongozo kwa Watazamaji wa Ndani na wa Kimataifa wa Uchaguzi ambao nimepewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Naahidi kuufuata na kwamba shughuli za utazamaji wa mchakato wa uchaguzi zitatekelezwa kwa ufasaha kwa namna Mwongozo ulivyoelekeza. Pia, natamka kwamba, sina maslahi binafsi ya kisiasa, kiuchumi au yoyote, ambayo yataingilia uwezo wangu wa kuwa mtazamaji wa uchaguzi asiye na upendeleo.

Jina:______________________________________________

Uraia: ____________________________________________

Shirika/taasisi: ___________________________________

Wadhifa: _________________________________________

Saini: ____________________________________________

Tarehe: __________________________________________

Dar es Salaam, DKT. WILSON MAHERA CHARLES
......................., 2020. *Mkurugenzi wa Uchaguzi*